# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 14 Safari ya jangwani – 1

**SOMA Kutoka 15:22 – 25; 16; 17:1 – 7; 32:1 – 8, 20 & 26**
**Hesabu 13:1 & 17 – 32; 14:1 – 4**

**SOMO**

Watu wa Israeli waliongozwa na Musa kupitia Bahari ya Shamu mpaka jangwa la Sinai. Watu hawa waliishi kwa mahema. Haukuwa muda mrefu hawa watu walisahau vile hawakutaka kuwa watumwa Misri. Walisahau vile Mungu aliwaokoa kwa kutuma Musa awaongoze na kuleta tauni kwa Wamisri halafu kuwavusha Bahari ya Shamu. Hawakupenda kuishi jangwani tena waliacha kuamini kwamba Mungu atawalinda. Walilalamika kwa sababu hakukuwa na chakula na maji.

Walinun'gunikia hapo Mara kwa sababu kulikuwa na maji yalikuwa chungu na Horebu hakukuwa na maji. Lakini Mungu aliwalinda. Kule Mara ,Mungu alifanya maji yakawa tamu. Na Horebu Mungu aliambia Musa apige mwamba kwa fimbo yake na maji yalitoka na watu walikunywa. Kulikuwa na wakati Mungu aliwapa ndege waitwao kware ili wale. Kila siku kwa miaka 40, Mungu aliwapa mikate isio ya kawaida kukula. Walipoamka asubuhi hizo mikate zilikuwa kila mahali na watu waliokota za siku moja na kukula. Hii mikate iliitwa *mana.* Siku ya Ijumaa, watu waliokota mana ya kutosha siku mbili na ilikuwa bado ni nzuri kukula Jumamosi – siku ya Sabato hawakutakiwa wafanye kazi.



Lakini bado watu walinun'gunika. Walikumbuka vitu vizuri walivyokuwa wakikula kule Misri: samaki, tikiti, aina ya vitunguu na vitunguu saumu – walinun'gunika kwa sababu walikula mana pekee yake.

Miezi mitatu baada ya kutoka Misri walifika Mlima wa Sinai. Walipiga kambi chini ya huo mlima. Mungu alikumbusha Musa kwamba Waisraeli ni watu wake wakipekee. Mungu alikuwa amewachagua kuwa watu wake alipoahidi Ibrahimu kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa.

**Maswali na Majibu**

1. Chakula chenye Mungu alileta kila siku kiliitwa nani? *Mana*
2. Musa alikuwa kwa Mlima wa Sinai kwa siku ngapi? *Siku 40.*
3. Watu walifanya nini Musa alipokuwa bado mlimani?
   *Walimshawishi Haruni kutengeneza ndama ya dhahabu iwe mungu wao.*
4. Kabila gani ilikuwa upande wa Mungu? *Lawi*
5. Musa alituma wapelelezi wangapi kwenda kuangalia Nchi ya Ahadi.
   *Wapelelezi 12*
6. Walirudi na matunda gani?
   *Kishada kubwa ya zabibu iliyobebwa na watu 2*
7. Wapelelezi walisema hiyo nchi ilikuwa ya namna gani?
   *Ilikuwa nchi nzuri yenye ilitiririka na maziwa na asali na chakula kingi na matunda*.
8. Mbona wapelelezi 10 walisema kwamba Waisraeli wasiende kwa hiyo nchi?
   Kwamba *miji ya kule ilikuwa na kuta na milango za nguvu, tena kulikuwa na majitu.*
9. Wapelelezi gani walikuwa na imani kwamba Mungu atakuwa nao?
   *Yoshua na Kalebu.*
10. Adhabu kwa Waisraeli ilikuwa gani kwa sababu ya kutokuwa na imani?
    *Watatangatanga jangwani kwa miaka 40.*

### Mistari ya kukariri

Hesabu 14:8; Zaburi 106:19 – 20 Yohana 6:32 – 33

### Mazungumzo

Soma Waebrania 3:9 – 14. Waisraeli walinun'gunika kila wakati. Zungumza juu ya mambo yaliyofanya Waisraeli wanun'gunike. Wangefanya nini? Zungumza vile tunaweza kufanya mambo yasipotuendea vizuri.

### Kuandika

Andika juu ya kilichofanyika Musa alipokuwa Mlima wa Sinai.

Mungu aliwapa Waisraeli sheria na maagizo mengi ili wamuheshimu na wawe watu wake. Mungu alimwambia Musa aende juu ya mlima ili ampe hizi sheria na maagizo. Kabla Musa hajaenda juu mlimani aliambia Waisraeli watii amri za Mungu wakati wote atakapokuwa kule mlimani. Musa aliambia Waisraeli kwamba wakiwa na shida yoyote, watamwendea Haruni awasaidie. Musa aliambia Waisraeli waabudu Mungu pekee vile walikuwa wameamriwa.

Mungu alizungumuzia Musa kule mlimani kwa siku arobaini. Mungu alimwambia amri zenye alitaka Waisraeli watumie. Mungu alielezea Musa vile alitaka Waisraeli wamwaabudu. Mungu alimpa Musa moyo (kumpa nguvu). Mungu aliahidi kuwaongoza na kuwasaidia jangwani. Tutajifunza mengi juu ya sheria na maagizo yenye Mungu alimpa Musa kwa somo lingine baadaye.



Wakati ule ule, kwa kambi ya Israeli hawakujua nini ilikuwa imefanyikia Musa. Musa alikuwa amekuwa kule kwa siku 40. Walifikiria alikuwa amekufia mlimani. Waisraeli walisahau juu ya Mungu. Hawangeweza kumuona Mungu na hawakujua penye Musa alikuwa. Walimwendea Haruni na kumwambia, “Ni muda mrefu tangu Musa aende mlimani. Hatujui nini imemfanyikia. Tutengenezee sanamu ili tumwabudu. Hatujui penye Mungu ako, na nini imefanyika kwa Musa. Tunataka mungu mwenye tunaona ili tumwaabudu.”

Haruni hakukuwa kiongozi wa nguvu tena mzuri kama Musa. Haruni aliogopa kwamba Waisraeli watamuua ikiwa hatawatengenezea sanamu. Haruni aliwambia wamletee vipuli vyao vya dhahabu vya masikio. Aliyeyusha hivyo vipuli vyo dhahabu. Kutoka kwa hiyo dhahabu alitengeneza ndama ya dhahabu. Akawambia hao watu, “Ndiyo huyu mungu wenu.” Waisraeli hawakuwa na imani. Walitaka mungu waliyemuona. Waliabudu mfano wa ndama badala ya Mungu Mwenyezi aliyeumba vitu vyote na aliyekuwa amewalinda na kuwaokoa kutoka Misri.

Waisraeli walitengeneza madhabahu na kuabudu ndama ya dhahabu. Walifanya maovu mengi. Walisema, “Huyu ndama ni mungu wetu aliyetuleta salama kutoka Misri. Lakini Musa hakuwa amekufa. Mungu aliona vile Waisraeli walikuwa wamemsahau haraka sana na kuabudu ndama ya dhahabu. Kwa hivyo Musa aliteremka kutoka mlimani.

Musa alikasirika sana alipoona Waisraeli wakiabudu ndama ya dhahabu. Wamisri waliabudu ndama ndume kama ishara ya nguvu. Lakini Musa alijua kwamba mfano ya ndama ya dhahabu haingewasaidia. Musa aliharibu hiyo ndama ya dhahabu.

Musa alikuwa na imani kwa Mungu aliyekuwa amefanya miujiza mingi huko Misri na alikuwa amewapa chakula na maji katika safari yao ya jangwani. Musa alipaza sauti, “Nani ako upande wa Bwana?” Kabila ya Lawi walikuja upande wa Musa na kusema, “Sisi tutaabudu Bwana.” Mungu alifurahi kuona kwamba kabila moja kwa kumi na mbili ya Israeli bado ina mpenda. Mungu akachagua kabila ya Lawi iwe ya makuhani Wake.

Waisraeli walitembea jangwani kwa miaka miwili. Baadaye walikuja kwa mpaka wa nchi ya Kanaani. Musa aliwakusanya Waisraeli wote pamoja. Aliwambia kwamba walikuwa wamefika kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi kuwapa. Wanatakiwa wawe na ujasiri na nguvu. Lazima waamini Mungu kwa sababu atawasaidia washinde nchi waendayo.

Musa alituma wapelelezi kumi na wawili yaani mmoja kwa kila kabila ya Israeli. Aliwambia watembee nchi yote ili waone vile ilivyo. Wapelelezi walitembea nchini kwote kwa siku arobaini. Waliona miji mikubwa yenye kuta za nguvu na milango kubwa. Waliona watu wa kule na baadhi yao wengine walikuwa majitu. Walipata matunda ya ajabu. Walirudi na kishada kimoja cha zabibu na kilikuwa kikubwa mpaka kilibebwa na watu wawili.

Wapelelezi walikuwa na mengi ya kusimulia. Walisema kwamba nchi ilikuwa nzuri sana – nchi yenye maziwa nyingi na asali. Ilikuwa nchi ya mazao mengi. Kulikuwa na mimea ya chakula na matunda mengi. Waisraeli walifurahia habari nzuri juu ya hiyo nchi. Lakini wapelelezi kumi hawakuamini Mungu. Walisema, “ Ni nchi nzuri ndiyo, lakini watu wanaoishi kule wana nguvu kukuliko sisi. Wengine ni majitu Watu wa kule wanaishi kwa miji mikubwa iliyo na kuta za nguvu na minara. Sisi tumeogopa kwenda kuishi kwa hiyo nchi. Hatutaweza kupigana na wale watu wa nguvu.”

Wapelelezi wawili, Yoshua na Kalebu, walikuwa waaminifu. Waliwambia Waisraeli kwamba, “Mungu ana nguvu kuliko majitu. Atatusaidia tuchukue hiyo nchi.” Lakini Waisraeli hawakusikiliza hayo. Walisahau miujiza yote yenye Mungu alikuwa amewafanyia. Waliamua kuchagua kiongozi mwingine na warudi Misri.

Halafu utukufu wa Mungu ulitokea kwa Maskani katikati ya kambi. Mungu aliwambia Waisraeli kwamba kwa sababu wameogopa na hawajamwamini, hatawakubali waende kwa nchi ya ahadi. Wapelelezi walichukua siku arobaini kupeleleza nchi. Mungu aliwambia lazima watarudi jangwani na waranderande kule kwa miaka arobaini. Kwa kila siku moja yenye wapelelezi walichukua kupeleleza nchi, Waisraeli watachukua mwaka mmoja jangwani. Hiyo ilikuwa adhabu kutoka kwa Mungu kwa sababu hawakumwamini.